

DAI HAKI ZAKO ZA MAJI, TIMIZA WAJIBU WAKO

Ulinzi dhidi ya maafa ya Mafuriko na Ukame

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasema kwamba lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi. Kwa mamlaka hayo, serikali ina wajibu wa kikatiba wa kuwalinda watu wake dhidi ya maafa kama vile mafuriko na ukame.

UKAME NA MAFURIKO

Sheria ya Kukabiliana na Maafa ya mwaka 2015 inataka uanzishwaji wa Kitengo cha Kukabiliana na Maafa katika ngazi za mkoa, wilaya, kata na kijiji. Sheria hiyo imeweka majukumu yafuatayo kwa kitengo hicho;

MAMLAKA ZENYE WAJIBU

Idara ya Kukabiliana na maafa

- Kuunda sera na mipango kuhusu shughuli za kukabiliana na maafa
- Kutengeneza mfumo wa kutoa taarifa za mapema kuhusu maafa kwa kuhusisha sekta zote.
- Kuandaa na kusimamia rasilimali kwa ajili ya shughuli za kukabiliana na maafa



Kamati za Mkoa za kukabiliana na maafa

Kamati hizi zina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za kupunguza hatari na kukabiliana na maafa na kuendesha shughuli za dharura za kukabiliana na maafa ikiwa ni pamoja na;

- Kukusanya na kusimamia rasilimali za kukabiliana na maafa katika ngazi ya mkoa.
- Kuandaa mfumo wa taarifa za mapema za maafa katika ngazi ya mkoa.


Kamati za Kukabiliana na maafa za Wilaya, zikiwa chini ya Wakuu wa Wilaya, zina majukumu yafuatayo:

- Kuunda na kutekeleza mipango ya maandalizi ya maafa ya wilaya na mipango ya kukabiliana wa maafa.
- Kusimamia shughuli zote za kukabiliana na maafa katika ngazi ya wilaya.



Kamati za kukabiliana na maafa ngazi za Kata na Vijiji/Mtaa

- Kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa na mipango ya dharura
- Kuunda na kuratibu mipango ya kupunguza na kukabiliana na athari za maafa, na mifumo ya taarifa za mapema.
- Kusimamia utekelezaji wa ukabilianaji wa maafa na programu za taarifa na uelewa kwa umma.



WAJIBU WAKO

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, na Sheria ya Kukabiliana na maafa ya mwaka 2015, kila mwananchi ana wajibu wa kulinda na kuboresha mazingira ili kupunguza hatari za maafa. Aidha;

- Wananchi wana jukumu la kutoa taarifa kwa mamlaka husika juu ya shughuli yoyote inayofanyika na inaweza kuathiri mazingira kwa kiasi kikubwa.
- Wananchi wana jukumu la kuonyesha utayari na nia ya kushiriki katika shughuli za kukabiliana na maafa.

Mawasiliano: Wasiliana na mamlaka husika kwa taarifa zaidi.

Ofisi ya Waziri Mkuu
Idara ya kukabiliana na Maafa
S.L.P . 980, DODOMA

Simu: 026 2322480 Barua pepe: ps@pmo.go.tz

Pia, unaweza kuwasiliana na mamlaka husika katika kila ya Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji au Mtaa popote pale Tanzania